



Ohio Statewide

Family Engagement Center

at The Ohio State University



## Mahudhurio: Muhimu kwa Mafanikio ya Mtoto Wako

### Kuhudhuria shule kunapelekea...

- Kuboresha ujuzi wa lugha ya Kiingereza haraka zaidi.
- Kupata marafiki zaidi shuleni na kujisikia kama sehemu ya jumuiya ya shule.
- Afya na ustawi bora.
- Kuhusika na shughuli zaidi za shule kama vile muziki, michezo, na vilabu vingine.
- Mahusiano ya karibu na walimu.
- Kuhitimu kwa wakati.
- Kujenga ujuzi muhimu kwa chuo au kazi za baadaye.

### Je, familia yako inaweza kufanya nini?

- Jadili na mtoto wako kuhusu manufaa ya kwenda shule kwa kina iwezekanavyo.
- Shirikiana na mtoto wako kufuatilia mahudhurio yake.
- Kuwa na ratiba ya kawaida nyumbani inayofanya iwe rahisi kwa mtoto wako kuhudhuria shule mara nyingi iwezekanavyo.
- Panga pamoja na mtoto wenu, familia au marafiki ili kumpeleka mtoto wenu shuleni kwa wakati.
- Omba usaidizi mkiwa na maswali na changamoto kuhusiana na mahudhurio. Shule ya mtoto wako inaweza kusaidia!
- Epuka kuratibu miadi au mipango wakati wa siku ya shule ya mtoto wako, isipokuwa ikiwa ni dharura.
- Uliza walimu wa mtoto wako jinsi mtoto wako anaweza kufidia masomo na kazi alizokosa.

### Ni wakati gani mtoto wako anapaswa kukosa shule?

- Kama ana homa ya nyuzijoto 101.4 au zaidi.
- Kama ametapika mara mbili zaidi katika kipindi cha saa 24 zilizopita.
- Kama ana matatizo ya kufika msalani kwa wakati.
- Kama kinyesi chake ni cha rangi ya manjano.

### Je, unajua kwamba?

Shule za Ohio hupima mahudhurio **kulingana na saa** ambazo mtoto yuko shuleni kila mwaka kutoka shule ya chekechea hadi kuhitimu. Ni muhimu kufika shuleni kwa wakati na kuepuka kuondoka kabla ya wakati. **Kila saa ni muhimu.**

**PATA MAELEZO ZAIDI**



Tembelea tovuti ya Kituo cha Ushirikishaji wa Familia cha Ohio Nzima:

[ohiofamiliesengage.osu.edu](http://ohiofamiliesengage.osu.edu)